

Jina.....

Nambari yako...../.....

Shule.....

Tarehe .....

Sahihi ya Mtahiniwa.....

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

(FASIHI)

JULAI / AGOSTI - 2012

MUDA: SAA 2 ½

## MTIHANI WA PAMOJA – WILAYA YA TESO KUSINI -2012

*Hati Ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Nchini Kenya*

### MAAGIZO

1. Jibu maswali **manne** pekee
2. Swali la kwanza ni la **lazima**
3. Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka **sehemu nne** zilizobaki ; yaani **Riwaya, na Hadithi fupi. Tamthilia, Fasihi Simulizi.**
4. Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja
5. Kila swali lina alama 20

*Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa  
Watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa*

## SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI

### Swali la lazima

1. a) Eleza namna amabavyo hachira wanahusishwa katika utambaji. Toa hoja nne. (ala. 8)
- b) Taja na ueleze sifa nne bainifu za hadithi. (ala.4)
- c) Fafanua sifa nne za fanani / mtambaji bora wa hadithi. (ala.8)

## SEHEMU B: TAMTHILIA: KIFO KISIMANI

### JIBU SWALI LA PILI ( 2) AU LA TATU ( 3)

2. I: Y : Utakuwa na Heshima kubwa katika Butangi  
II Y: Utakuwa na mali,mali tele. Mali inayostahili jina mali
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (ala. 4)
- b) Taja ‘mali’ ambayo angemiliki anayezungumziwa. (ala. 4)
- c) Bainisha mbibu kuu ya uandishi inayotawala dondoo hili. Thibitisha jibu lake. (ala. 2)
- d) Vijana wamesawiriwa vipi katika tamthilia ya kifo kisimani ? (ala. 10)
3. Fafanua kwa tafsili dhiki zinazowakumba wana-Butangi. (ala. 20)

## SEHEMU C : RIWAYA UTENGANO

### JIBU SWALI LA 4 AU LA 5

4. Eleza jinsi maudhui yafuatayo yanavyojitokeza katika Riwaya ya utengano.
  - a) Unafiki (ala. 10)
  - b) Kisasi (ala. 10)
5. “Msiba wa kujitakia hauna kilio” Onyesha ufaafu wa methali hii kwa kurejea riwaya ‘Utengano’ (ala. 20)

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

6. **Mwanaume amesawiriwa vipi katika hadithi zifuatazo?**

- a) Ngome ya nafsi . (ala. 5)
- b) Kachukua Hatua nyingine (ala.5)
- c) Mayai waziri wa maradhi . (ala.5)
- d) Uteuzi wa moyoni. (ala.5)

## SEHEMU E : USHAIRI

**Soma shairi kisha uyajibu maswali**

Chema hakidumu, kingapendekeza  
Saa ikitimu, kitakuteleza,  
Ukawa na hamu, kuingojeleza,  
Huwa ni vigumu, kamwe huitaweza  
Chema sikiimbi, kwamba nakitweza,  
Japo mara tumbi, kinshaniliza  
Na japo siombi, kipate n'ongeza  
Mtu huniambi, pa kujikimbiza

Chema mara ngapi, kinaniondoka,  
Mwanangu yu wapi ? Hakukaa mwaka,  
Kwa muda mfupi, aliwatilika  
Ningefanya lipi, ela kumzika

Chema wangu babu, kibwana bashee,  
Alojipa tabu, kwamba anilee,  
Na yakwe sababu, ni nitengenee,  
Illahi wahhabu, mara amtwee

Chema wangu poni, kipenzi nyanyangu,  
Hadi siku hini, yu moyoni mwangu  
Yu moyoni ndani, hadi kufa kwangu  
Ningamtamani, hararudi kwangu

### Maswali

- a) Eleza dhamira ya mwandishi . (ala. 2)
- b) Fafanua umbo la shairi hili. (ala.4)
- c) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha nathari. (ala.4)
- d) Taja mbibu nne za uhuru wa mshairi kwa kutolea mifano mwafaka. (ala.4)
- e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (ala.6)
- f) i) Nitengenee  
ii) Ningamtamani  
iii) Ikitimu